



ST. FRANCIS UNIVERSITY COLLEGE OF HEALTH AND ALLIED SCIENCES



A Constituent College of St. Augustine University of Tanzania

P.O. Box 175

Phone: (255) 23-2931-568

Email: principal@sfuchas.ac.tz

Ifakara, Tanzania

Fax: (255) 23-2931-569

Website: www.sfuchas.ac.tz

TANGAZO LA UDAHILI KWA KOZI ZA AFYA MWAKA WA MASOMO 2021/2022

Mkuu wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Tiba cha Mtakatifu Francisco (St. Francis University College of Health and Allied Sciences) kilichopo Ifakara, Morogoro anapenda kuutarifu umma kuwa UDAHILI kwa kozi za afya mwaka wa masomo 2021/2022 utaanza tarehe **17/9/2021 hadi tarehe 30/9/2021** kwa kozi zifuatazo:

1. Stashahada ya Ufamasia
2. Stashahada ya Maabara
3. Kozi ya Udakitari wa binadamu, dirisha litafunguliwa kuanzia tarehe **18/9/2021** hadi tarehe **24/9/2021**

SIFA ZA MWOMBAJI

Sifa za waombaji wa kozi ya Ufamasia:

Mwombaji awe alihitimu kidato cha nne na kupata ufaulu usiopungua alama "D" katika masomo manne yasiyo ya dini ikiwemo **Biolojia** na **Chemia**.

Sifa za mwombaji wa kozi ya Maabara:

Mwombaji awe alihitimu kidato cha nne na kupata ufaulu usiopungua alama "D" katika masomo matano yasiyo ya dini ikiwemo Biolojia, Chemia, na Fizikia/Engineering. Ufaulu katika masomo ya Hisabati na Kingereza itakua ni sifa ya ziada.

Sifa za waombaji wa kozi ya Udakitari wa binadamu:

1. Kwa muhitimu wa kidato cha sita awe na ufaulu usiopungua alama "D" katika masomo ya **PHYSICS, CHEMISTRY, na BIOLOGY**. Muhitimu anapaswa kuwa na pointi zisizopungua **6.0** katika masomo yote matatu.
2. Na kwa mwombaji mwenye Stashahada ya utabibu awe alihitimu kidato cha nne na kupata ufaulu usiopungua alama "D" katika masomo matano yasiyo ya dini. Mwombaji anapaswa kuwa na Stashahada ya utabibu yenye ufaulu usiopungua wastani wa "B" au GPA ya **3.0**.

Maombi yatumwe kupitia tovuti ya chuo <https://oas.sfuchas.ac.tz> au www.sfuchas.ac.tz – ONLINE APPLICATION

Kutokana na kuwa na kipindi kifupi cha udahili, waombaji wanashauriwa kutuma maombi yao haraka iwezekanavyo.

Nb: Hakuna gharama ya kutuma maombi kwa waombaji wa stashahada ya Ufamasia na Maabara

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kwa simu 0658 592 300 au 0769 810 317, Au kwa barua pepe: admission@sfuchas.ac.tz, Au fika chuoni St. Francis University College, Ifakara.